

**SHIRIKA LA TAIFA LA HIFADHI YA JAMII
(NSSF)**



**KIKAO CHA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA SHIRIKA
LA TAIFA LA HIFADHI YA JAMII NA HESABU
ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA
2014/2015**

TAREHE 24 OKTOBA, 2016

TAARIFA FUPI YA UTENDAJI KAZI WA SHIRIKA LA HIFADHI YA
JAMII (NSSF) NA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA KIPINDI CHA
MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mh. Aeshi Halfani Hilaly (Mbunge)

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC),

*Waheshimiwa Wajumbe wa kamati ya Kudumu ya Bunge
ya Hesabu za Serikali.*

1.0 Utangulizi

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima ya kuwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii – NSSF kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 na hesabu zilizokaguliwa na Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kwa kushirikiana na Kampuni ya Ukaguzi ya Ernst & Young (EY). Taarifa hii inajumuisha pamoja na mambo mengine, hali ya utendaji kazi wa NSSF, mafanikio, changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii – NSSF lilianzishwa Julai, 1998 likichukua nafasi ya Shirika la Taifa la Akiba ya Wafanyakazi – NPF kufuatia kupitishwa kwa Sheria Na.28 ya mwaka 1997 na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.0 Madhumuni ya kuanzishwa kwa NSSF

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuanzishwa kwa NSSF ni kama yafuatayo:-

- (a) Kuandikisha wanachama na waajiri wanaotakiwa kujiunga na mpango wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii;
- (b) Kukusanya michango kutoka kwa waajiri walioandikishwa;
- (c) Kuwekeza fedha zilizokusanywa katika vitega uchumi vilivyo na usalama/uhakika wa kuleta faida;

- (d) Kuwalipa wanachama mafao yao wakati watakapotahiti kama ilivyoielezwa kwenye sheria; na
- (e) Kutoa ushauri kwa Senkati ili kuboresha masuala ya Hifadhi ya jamii Tanzania.

3.0 Mafao chini ya sheria ya NSSF

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao yanayotolewa chini ya NSSF yamegawanyika katika mafungu mawili ambayo ni mafao ya muda mrefu na yale ya muda mfupi.

- (a) Mafao ya muda mrefu yanalipwa kwa wanachama kwa mtindo wa pensheni nayo ni:-
 - (i) Pensheni ya uzee ambayo hulipwa kwa mwanachama aliyestaafu na kutimiza masharti yanayohitajika;
 - (ii) Pensheni ya ulemavu ambayo hulipwa kwa mwanachama ambaye atakuwa amepoteza uwezo wa kujitafutia kipato kutokana na ulemavu wa mwili au akili, na
 - (iii) Pensheni ya urithi ambayo hulipwa kwa waliokuwa wakimtegemea mwanachama aliyefariki wakati akiwa bado katika ajira.
- (b) ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kuhusu mafao ya muda mfupi, mafao haya hulipwa kwa vipindi vya muda mfupi na kwa muda maalum kama ilivyoainishwa katika sheria.

Mafao haya ni manne nayo ni:-

- (i) Msaada wa mazishi ambao hutolewa kwa pesa taslimu kwa mtu aliyegharamia mazishi ya mwanachama aliyefariki;
- (ii) Mafao ya uzazi ambayo hutolewa kwa mwanachama mwanamke kabla na baada ya kujifungua. Mafao ya uzazi yanajumuisha

kupaliwa matibabu na fedha fedha na hutolewa kwa mwanachama kila baada ya maka mitalu,

- (iii) Mafao ya kuumia kazini ambayo hutolewa kwa mwanachama ambaye ameumia kutokana na kazi anayoifanya au kupata ugonjwa uliosababishwa na kazi yake; na
- (iv) Mafao ya malibabu ambayo yanahusu huduma za matibabu kwa mwanachama na familia yake inayojumuisha mke au mume wa mwanachama na watoto wao wasiozidi wanne kwa magonjwa yote isipokuwa yale yanayotibiwa na mipango ya taifa kama vile UKIMWI, Saratani, kifua kikuu n.k.

4.0 Malengo ya mwaka 2014/2015

4.1 Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika lililenga kutekeleza yafuatayo:-

- (a) kukusanya michango kutoka kwa waajiri na wanachama inayofikia shilingi milioni 1,012,354.1 na mapato yatokanayo na vitega uchumi (Investment income) kiasi cha shilingi milioni 209,689.0;
- (b) kutoa elimu kwa wanachama wake, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo wa Hifadhi ya Jamii; kupima afya za wanachama wake (Preventive Health Checks) na kufanya mkutano mkuu wa tano wa wadau wa NSSF;
- (c) kulipa mafao kwa wanachama wake yanayofikia shilingi milioni 219,999.8;
- (d) kukamilisha tathimini ya uwezo wa mfuko kifedha ili kulipa mafao kwa wanachama wake kwa muda mrefu ujao;
- (e) kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigamboni;

(f) Kukamilisha ujenzi wa vilega uchumi katika mkoa ya Chinyanga, Morogoro, Kilimanjaro, NSSF/RITA "Complex", Wilaya ya Itala na mradi wa nyumba za bei nafuu mia nane Mtoni Kijichi awamu ya Tatu. Pia kuendelea na ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu "Farm" - "Satellite cities"), na ujenzi wa Jengo la Mzizima Towers jijini Dar Es Salaam.

(g) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Appolo, ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni ("~~Azimio Satellite town~~" na Geza Satellite Town), ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma (MP's Village), Ujenzi wa Majengo ya NSSF/Maadili, NSSF/TBC, NSSF/NIP.

5.0 Hali ya Utendaji kazi 2014/2015

5.1 **Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, utendaji wa kazi katika Shirika la NSSF ulikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mapato

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika lilikusanya kiasi cha shilingi milioni 605,090.0 kutoka kwa waajiri ukilinganisha na shilingi milioni 548,471.6 zilizokusanywa mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko la 10%. Lengo la makusanyo ya michango kwa mwaka huo lilikuwa kukusanya shilingi milioni 1,012,354.1; hivyo kuwa na upungufu wa 40% kufikia lengo.

(b) Malipo ya Mafao

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika limelipa mafao kwa wanachama wake yanayofikia shilingi milioni 357,672.7 ikiwa ni ongezeko la 3.74% ukilinganisha na mafao ya shilingi milioni 344,787.05 yaliyolipwa mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha lengo la kulipa mafao ya jumla ya shilingi 219,999.60 mwaka huo lilivukwa kwa 63%.

(c) Gharama za Uendeshaaji

Gharama za kuendesha Shirika (Administrative costs) zilikuwa shilingi milioni 110,260 ukilinganisha na shilingi milioni 105,224 mwaka 2013/2014. Makisio ya gharama za uendeshaaji kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 ilikuwa shilingi 118,128.4 Gharama halisi ukilinganisha na makisio ya mwaka 2014/2015 ni 6.66%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuirifu Kamati yako kuwa kwa mara nyingine tena Shirika limeweza kudhibiti matumizi ambayo yalifikia 13.80% ya mapato ya Shirika kwa kipindi hicho. Kiwango hiki kinakidhi mahitaji ya kifungu Namba 6i (4) cha Sheria ya NSSF ambacho kinatamka wazi kuwa kwa vyo vyote vile matumizi ya Shirika yasizidi 15% ya mapato.

(d) Kukua kwa Mfuko

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilega uchumi vya Shirika (Investments) vimeongezeka kutoka shilingi milioni 2,403,606 hapo Juni, 2014 na kufikia shilingi milioni 2,726,013.5 ilipofika Juni, 2015. Hii ikiwa ni ongezeko la 13.41% Lengo lilikuwa kufikia shilingi milioni 2,956,440.04 hapo Juni, 2015. Hivyo matokeo yalikuwa ni 92.21% ya lengo.

Kwa ujumla Mfuko umeongezeka kutoka thamani ya shilingi milioni 2,582,920.8 hapo Juni, 2014 hadi kufikia shilingi milioni 2,933,972.03 ilipofika Juni 2015. Hili ni ongezeko la 13.60%.

Awali ilikadiriwa kuwa thamani ya Mfuko (Total Assets) ingefikia shilingi milioni 3,711,411.50 Juni, 2015. Ikilinganishwa na hali halisi ya Mfuko ilipofikia tarehe 30 Juni, 2015, thamani ya Mfuko ilifikia 84.40% ya lengo.

(e) Uandikishwaji wa Wanachama

Mpaka kufikia Juni 2015, idadi ya wanachama ilikuwa na kufikia 665,710 ikilinganishwa na wanachama 567,109 kwa kipindi kilichoishia

wa Juni 2014. Hili ni sawa la ongezeko la asilimia 1/4. Ongezeko hilo lilichangiwa na elimu iliyotolewa kwa wanachama kupitia vyombo vya habari na semina mbali mbali, ambapo semina 4,078 zimetolewa kwa waajiri na wanachama nchi nzima. Vile vile Shirika lilifanya Mkutano Mkuu wa Tano wa Wadau wa NSSF mwezi Juni, 2016 ambao ulihudhuriwa na Watu 800.

(f) Hali ya Ukwasi ya Shirika (Liquidity)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, hali ya Ukwasi haikuwa nzuri sana ambayo ilisababisha Shirika kushindwa kufanya malipo mbalimbali kwa wakati, hasa zaidi malipo ya wakandarasi.

(g) Tathmini ya muda mrefu ya Mfuko (Acturial Valuation)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya muda mrefu ya Mfuko yaani "Acturial Valuation" inayoishia mwezi Juni, 2013, ilifanywa na International Labour Office ("ILO"). Thathmini hiyo imeonyesha kuwa hali ya kifedha ya NSSF in imara (Solvency); kwa maana ya uwezo wa kulipa mafao kila mwanachama mwenye sifa kwa zaidi ya miaka 50 ijayo bila kutetereka.

Uwezo huu wa kifedha unapimwa kwa kuangalia uwiano wa akiba (Reserve) iliyopo na matumizi ya Mfuko katika kulipa mafao ya wanachama na gharama za uendeshaji. Kipimo hiki kinaonyesha idadi ya miaka ambayo Mfuko unaweza kulipa mafao ya wanachama na kumudu gharama zote za uendeshaji bila kukusanya cho chote.

Ili mfuko uonekane kuwa uko imara unatakiwa angalau uwe na "Reserve ratio" ya 3 ndani ya miaka 20 tangu tarehe ya tathmini. Matokeo yanaonyesha Reserve Ratio ya NSSF kwa 2008/09 ni 6.6. na 2028/29 ni 3.6.

Tafiti ya matokeo haya ni kwamba, kwapo NSSF itasitisha kukatana michango sasa inaweza kulipa mafao pamoja na gharama za uendeshaji kwa miaka 7 bila kutetereka. Uwezo huu kwa miaka 20 itayo utakuwa kwa miaka 4 ambayo ni juu ya kiwango cha miaka 3 inayotumika kupima uwezo wa kifedha wa mfuko.

Tathmini nyingine ya muda mrefu (actuarial valuation) inatarajia kufanyika kuanzia 1 January 2017 na kukamilika 31 May 2018. Tathmini hii itafanywa tena na wataalamu toka International Labour Office ("ILO") na watatoa tathmini ya mfuko itakayoishia 30 June 2016. Maandalizi ya ukusanyaji wa takwimu yameshaanza.

Tathmini za muda mrefu (actuarial valuation) hufanywa kila baada ya miaka mitatu. Ila mfuko upo katika mikakati ya kuweza kufanya tathmini kila mwaka kwa kutumia wataalam wetu wa ndani pamoja na wataalam kutoka International Labour Office ("ILO")

(h) Utekellezaji wa Miradi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika limepata mafanikio makubwa katika kutekeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo;

(i) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni ilikamilika mwezi Machi 2016. Mradi huu ulijumuisha ujenzi wa barabara zinazoliunganisha daraja hilo na upande wa Kurasini, ambapo hadi sasa shilingi bilioni **264.42** zimetumika. Kwa sasa hivi, kazi iliyobakia ni ujenzi wa barabara za maungio kuelekea Kigamboni, ambapo hadi vii sasa mradi huko katika hatua ya mchakato wa malipo ya fidia kwa wanachi watakoathirika na mradi, ambapo uhakiki wa watu watakoalipwa umekamilika.

(ii) Ujenzi wa majengo ya vitega Ofisi na vitega Uchumi katika Mikoa ya Shinyanga, Morogoro, NSSF/RITA "Complex", yamekamilika. Aidha, Ujenzi wa Jengo la Kitega katika Wilaya ya Ilala - Mzizima (EX -

Araco) ghorofa 35 unaendelea na kutarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2017/18

(iii) Ujenzi wa nyumba mia nane(800) za bei nafuu mtoni kigchi unaendelea na kati ya nyumba hizo, 720 ni za ghorofa na 100 ni nyumba zinazojitegemea ("massionettes"). Ujenzi wa nyumba hizi umefikia hatua ya asilimia 73%. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2016.

(iv) Ujenzi wa nyumba katika Vijiji vya kisasa Kigamboni; Tuangoma nyumba 131 na Dungu "Farm" nyumba 439 unaendelea na ulitarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2015/16. Hata hivyo, hadi leo tunapotoa ripoti hii, ujenzi umefikia asilimia 50% na shilingi bilioni 45.6 zimetumika.

(v) Ujenzi wa nyumba katika Kijiji cha kisasa Kigamboni kwa njia ya ubia; Mradi huu ni ubia kati ya NSSf na Kampuni ya Azimio Housing Estates Co.Ltd (AHEL), wenye kuhusisha ujenzi wa jumla ya nyumba 7,460 zilizotarajiwa kukamilika mwezi juni, 2017 umesimama. Ambapo hadi taarifa hizi zinawasilishwa majengo ya awali ("structures") 83 yenye nyumba 3,570 yameshajengwa na jumla ya Shilingi Bilioni 219.62 zimewekezwa na Shirika katika mradi huu. Shirika linafanya mazungumzo na mbia huyu ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili. Majadiliano haya yanahusisha pia kutathimini upya Mkataba wa Ubia uliokuwa umeingiwa kati ya pande zote mbili.

(vi) Ujezi wa Hoteli ya Kisasa nyota Tano Mwanza, unaendelea na unatarajiwa kukamilika Mwezi Novemba 2017. Hoteli itakuwa na vyumba 200 vya ukubwa mbalimbali pamoja na chumba kwa matumizi ya rais, pia kutakuwa na ukumbi mkubwa na wa kisasa wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 500, mabwawa ya kuogelea na schemu za kutosha za kuegesha magari. Hadi hivi sasa ujenzi umefikia asilimia 51.5.

- (vii) Mradi wa Kliniki ya Kisasa cha Uchuguzi wa Magonjwa (NSSF Apollo Diagnostic Clinic), Umesiamia.

Lengo la Mradi huu, ni ujenzi wa kituo cha tiba (Kliniki) kwa ajili ya kutathmini na kutibu magonjwa mbali mbali. Kituo hiki ilitegemea kupunguza gharama kwa wataanzania na majirani zetu katika nchi za maziwa makuu kwa kutoa huduma mbali mbali ikiwemo ya moyo na kansa ambazo sasa watu wengi wamekuwa wakifuata ibi hizo India kwa gharama kubwa na muda mwingi. Kliniki hii ilikuwa imilikiwe kwa ubia kati ya NSSF na Hospitali ya Apollo ya India ambapo Apollo walipaswa kuleta wataalam na kuendesha kliniki hiyo Mradi huu lengounaendelea na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/16.

Mradi huu umesimama kwa sasa ambapo thathimini ya kina juu ya fedha zilizotumika unafanyika ili kutambua kama fedha zilizotumikazinaendana matarajio ya thamani ya matumizi hayo (Value for Money). Uendelezaji wa mradi huu utafanyika mara baada ya thamini hiyo kukamilika.

- (viii) Aidha miradi ya ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma (MP's Village), ujenzi wa Majengo ya NSSF/Maadili, NSSF/TBC, NSSF/NIP imeshindikana kuanza kutokana na kutopatikana kwa dhamana kutoka Serikalini.

6.0 Changamoto

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, Shirika linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (a) Baadhi ya Waajiri kutowasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa wakati kwa viwango vinavyotakiwa;

- (b) Upatikanaji wa Hati za Kumiliki ardhi kwa viwanja vya vilega uchumi na maofisi umeendelea kuwa ngumu. Aidha ubadilishaji wa majina kwenye hati za viwanja vilivyotumuliwa na Shirika bado una matatizo.
- (c) Uelewa mdogo wa dhana ya Hifadhi ya Jamii miongoni mwa umma; na
- (d) Ongezeko kubwa la mafao ya kuacha uanachama (withdrawal) jambo ambalo linasababisha wastaafu miaka ijayo kukosa sifa ya kupata pensheni. Tatizo hili linaweza kuleta athari kubwa kwa maendeleo ya nchi yetu kwani Taifa litakuwa na idadi kubwa ya wazee ambao hawana kipato chochote.
- (e) Shirika limekutana na tatizo la kushindwa kulipa malipo mbalimbali hasa ya wakandarasi kwa wakati uliotakiwa kulipa.

7.0 Ufumbuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika limeendelea kutafuta ufumbuzi wa matatizo na changamoto mbali mbali na hatua zinazochukuliwa ni pamoja na:-

- (a) Shirika linaendelea na jitihada za kuelimisha waajiri juu ya umuhimu wa kuwasilisha michango sahihi na kwa wakati. Semina 4,078 za kuelimisha waajiri na wanachama zimefanywa katika mwaka 2014/15. Shirika limekuwa likitumia Radio na Television kutoa elimu kwa umma kuhusu maana ya Hifadhi ya jamii na mafao yatolewayo na Shirika.

Aidha Shirika limekuwa likichukua hatua za kisheria kwa wale waajiri wakorofi kwa kuwapeleka mahakamani. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, lilikuwa na jumla ya kesi 192 za thamani ya shilingi milioni 7,006.7. Ambapo Shilingi 523.0 milioni zilipatikana kutokana na kushinda kesi 19. Na kesi 56 za thamani ya shilingi milioni 3,419.03 zilikuwa zikiendelea mahakamani.

- (b) Shirika limeteua wataalam kufuatilia upatikanaji wa Hati za Kumiliki ardhi kwa viwanja vyote vya Shirika visivyo na hati nchi nzima.

- (c) Shirika limeendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Azma kuhabari kwa Shamba ya Hifadhi ya Jamii mawakebeshwari ili kupata ubandaji wa ongezeko la wamachuma wamioptoa wakiwa katika njia ili kutoa thamani mafao yao ya pandeni watakapofika wakati wa kustaifu.
- (d) Shirika litafanya miradi ambayo litaweza kukabiliana nayo kikamilifu. Na pia Shirika limeanza na litamarisha uwekezaji wa muda mrefu ("Fixed Deposit and Treasury Bills") ili kuweza kukabiliana na hali ya ukwasi.

8.0 Hitimisho

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hapo juu nina heshima kuibwa kuwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha Wizara, Bodi na Menejimenti ya NSSI sasa zipo tayari kupokea ushauri na maagizo ya Kamati yako.

Naomba kuwasilisha.



Prof. Godius Kahyarara
MKURUGENZI MKUU,
SHIRIKA LA TAIFA LA HIFADHI YA JAMII (NSSF)